

**“KUTENDANA”**

1. Niufungue mfundo, niloutunga sana  
Haufanguki kwa nyundo, ya utunzi wenye kina  
Kutaeda ni kutendana, tenda na mimi nitende  
Nyege ni kunyegezana, nyegeza nikunyegeze.
2. Nipa na mimi nikupe, kupana ni kupeana  
Leo nasema kweupe, si usiku ni mchana  
Ni kwa vyangu unenepe, hutaki kugawizana  
Nyege ni kunyegezana, nyegeza nikunyegeze.
3. Nyegeza nikunyegeze, nyege ni kunyegazana  
Wataka nikunoneze, hutaki kunonezana  
Nikisema nipuuze, vipi mwanzangu wanuna!  
Gawa ni kugawiana, gawa na mimi nigawe.

*Amiri A. S Andanenga,  
S.L.P 4775  
Kinondoni Shamba, Dar es Salaam*